USAID FROM THE AMERICAN PEOPLE

CDC

U.S. President's Malaria Initiative



# PRESIDENT'S MALARIA INITIATIVE TANZANIA

Tanzania Bara, zaidi ya asilimia 16 ya ziara zote za wagonjwa wa nje zinatokana na malaria, na kusababisha takribani visa milioni 7 vilivyothibitishwa kila mwaka. Asilimia 93 ya watu katika Tanzania bara wanaishi katika maeneo ya ugonjwa wa malaria, ugonjwa huu unabakia kuwa mchangiaji mkubwa wa vifo vya akina mama, watoto wachanga, na vifo vya watoto chini ya miaka mitano.

Mfuko wa Rais wa Marekani wa Kupambana na Malaria (PMI) unajitahidi kupunguza vifo vya malaria na kupunguza kwa kiasi kikubwa maambukizi ya malaria na lengo la muda mrefu la kutokomeza malaria. Kwa msaada kutoka kwa PMI na washirika wake, hatua za kudhibiti malaria zinaongezwa na bidhaa muhimu zinasambazwa kwa watu walio katika mazingira hatarishi. PMI hutumia njia jumuishi inayosisitiza kuzuia maambukizi kupitia vyandarua vyenye dawa (ITNs), kunyunyizia dawa za ukoko, na kuzuia malaria wakati wa ujauzito. Udhibiti wa magonjwa pia unasisitizwa kupitia utambuzi wa haraka na matibabu sahihi, kuimarisha ufuatiliaji wa malaria, kukuza uwezo wa rasilimali watu, na kukuza mienendo mema ya kuzuia malaria na usimamizi wa visa vipya.

Ufadhili wa hivi karibuni wa PMI Tanzania bara umejumuisha:

- Kunyunyizia dawa za ukoko kwa takribani nyumba 430,000 kwa mwaka 2019/2020 na kuwalinda watu zaidi ya milioni 1.6;
- Manunuzi ya vyandarua vyenye dawa zaidi ya milioni 3.1 mwaka 2019;
- Usambazaji wa vyandarua vyenye dawa zaidi ya milioni 3.1 kwa watoto wa shule za msingi za serikali katika mikoa kumi na nne ambayo ina maambukizi mengi ya malaria kwa mwaka 2019/2020;
- Iliendelea kusaidia usambazaji wa vyandarua vyenye dawa vilivyonunuliwa na Global Fund kwenda vituo vyote vya afya vya umma katika mikoa kumi na nne kwa mwaka 2019. Hivi vyandarua vyenye dawa hutolewa kwa wajawazito katika ziara yao ya kwanza wakati wa ujauzito, na pia watoto kwenye chanjo yao ya kwanza ya surua; na
- Iliendelea kusaidia na kuimarisha utekelezaji wa huduma za afya zinazofanya utabibu na matibabu ya malaria pamoja na uboreshaji wa utoaji taarifa sahihi katika mikoa kumi na moja yenye maambukizi mengi ya malaria.

Zanzibar, ufadhili wa hivi karibuni wa PMI umejumuisha:

- Kunyunyizia dawa ya ukoko kwenye nyumba 44,500 kwa mwaka 2020, ambayo imelinda zaidi ya watu 225,000;

- Ununuzi pamoja na usambazaji wa vyandarua vyenye dawa 288,000 kupitia kliniki za wajawazito, kliniki za chanjo, na njia zingine za jamii; na
- Iliendelea kushirikiana na Kitengo cha Kumaliza Malaria Zanzibar (ZAMEP) kudhibiti malaria, pamoja na ufuatiliaji ulioimarishwa kupitia kugundua kesi mapema na kutuma taarifa fupi kwa njia ya simu

Tanzania nzima, PMI inaendelea kusaidia ufuatiliaji wa magonjwa, mfumo wa afya na ugavi, usimamizi bora wa kesi za malaria, na utumiaji wa vyombo vya habari na mawasiliano kati ya watu ili kuboresha mienendo bora ya afya.

## MUHTASARI WA PMI

### KIWANGO CHA UFADHILI

- Dola za Marekani kwa Mwaka wa Fedha 2019

### WASHIRIKA WAKUU

- Mpango wa Taifa wa Kudhibiti Malaria
- Mpango wa Kutokomeza Malaria Zanzibar
- Taasisi ya Kitaifa ya Udhibiti wa Tiba
- VectorLink, Abt Associates Inc.
- Tanzania Vector Control Activity, Johns Hopkins University
- Boresha Afya, Lake and Western Zones, Jhpiego
- Boresha Afya, Southern Zone, Deloitte Tanzania
- Impact Malaria, PSI
- Malaria Indicator Survey, ICF Macro
- Digital Square, Path
- Peace Corps

### WAFADHILI WASHIRIKA

- The Global Fund
- Swiss Agency for Development and Cooperation (SDC)
- Shirika la Afya Duniani

### MAWASILIANO

Naomi Serbantez
nserbantez@usaid.gov

Dr. Erik Reaves
ereaves@cdc.gov

### TOVUTI

www.pmi.gov

## CHANGAMOTO

Juhudi za kuzuia na kudhibiti malaria ni ngumu na zinapata changamoto kutokana na upungufu wa rasilimali watu, ikiwemo watumihsi hususani katika ngazi ya wizara na ukosefu wa maafisa wa malaria wenye mafunzo, na upungufu wa wafanyakazi. Usimamizi dhaifu wa mnyororo wa usambazaji katika afya pia unachangamoto ya usimamizi wa hatua za matibabu na kinga katika vituo vya kitaifa. Uwezo wa kufuatilia na kupima malaria pia umepunguzwa na mifumo dhaifu ya taarfa. PMI inasaidia na kujenga juu ya mifumo ya afya ya USAID kuimarisha juhudi za kushughulikia masuala haya.

## MATOKEO

Michango ya PMI nchini Tanzania tangu 2005 ni pamoja na:

- Ununuzi wa dawa za matibabu milioni 43 wa dawa za kupambana na malaria ya artemisinin (ACT);
- Unyunyizaji wa dawa za ukoko majumbani kila mwaka, kulinda karibu watu milioni 2 katika duru ya hivi karibuni iliyokamilika ya unyunyizi (2019);
- Ununuzi wa ITN zaidi ya milioni 14; na
- Ununuzi wa zaidi ya vipimo milioni 19.4 vya uchunguzi wa malaria.

Kuongezeka kwa hatua za kuzuia na matibabu ya malaria kulingana na mikakati ya PMI, ZAMEP, na Programu ya Kitaifa ya Kudhibiti Malaria imeleta matokeo makubwa, pamoja na:

- Kupungua kwa maambukizi ya malaria hadi asilimia 0.2 kwa watoto chini ya miaka mitano huko Zanzibar. ZAMEP sasa imezingatia uondoaji wa mapema;
- Kuongezeka kwa idadi ya watoto chini ya miaka mitano wanaopata ACTs ndani ya masaa 24 ya kupata homa kutoka asilimia 14 hadi asilimia 60;
- Ongezeko la idadi ya kaya zinazomiliki angalau chandarua kimoja chenye dawa kutoka asilimia 38 mwaka 2007 hadi asilimia 77 mwaka 2017: na
- Katika kaya zilizo na angalau chandarua chenye dawa kimoja, asilimia 54 ya wajawazito na Watoto chini ya miaka mitano waliripoti kulala kwenye chandarua chenye dawa usiku uliopita mwaka 2017.